



SHIRIKA LA TIJA LA TAIFA

KOZI YA WASAIDIZI WA OFISI HATUA YA KWANZA

Malengo ya Kozi

Kuwaongezea washiriki ujuzi utakaowawezesha kuongeza ufanisi mahala pa kazi.

Walengwa

Wasaidizi wa Ofisi, wapokeaji wageni na wapokeaji simu.

Mada Muhimu

Muundo mahali pa kazi; Kazi na taratibu za ofisi; Mawasiliano bora kazini; Ufanisi na tija kazini; Wajibu na majukumu ya wasaidizi wa ofisi; Mapokezi ya wageni; Kuhudumia wateja; Uwajibikaji kazini; Kazi na taratibu za masijala; Uandishi wa barua za kikazi; Nidhamu kazini; Maadili ya kazi; Kuyamudu mabadiliko; Matumizi mazuri ya muda wa kazi; Ulinzi mahali pa kazi; Matumizi mazuri ya simu; Utunzaji wa vifaa vya kazi; Uandishi wa ripoti; Mahusiano katika ofisi; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Na. 6 ya mwaka 2004) na Sheria katika utumishi wa umma ya mwaka (2002); Afya ya mfanyakazi (ufahamu kuhusu HIV/AIDS na magonjwa mengine).

Matarajio

Baada ya mafunzo haya, washiriki wanatarajiwa kuongeza ujuzi wakatiwakitekeleza kazi na majukumu yao mahala pa kazi.

Mbinu za Mafunzo

Mchanganyiko wa Mafunzo kwa njia ya video, mazoezi kwa vikundi, Uwasilishaji wa mada, mazoezi kwa vitendo.

Lugha ya Mafunzo

Kiswahili

Tarehe

Kundi	Kuanza	Kumaliza
Moja	12 Agosti, 2019	30 Agosti, 2019
Mbili	09 Machi, 2020	27 Machi, 2020

Mahali

Morogoro – Kituo cha Tushikamane

Muda

Wiki tatu

Ada na Utaratibu wa Malipo

Ada ni Tshs. **1,110,000/=** na inatakiwa ilipwe kabla ya kuanza kozi kupitia akaunti ya Shirika la Tija la Taifa kwenye Benki ya CRDB, Namba ya Akaunti 01J1042999200, Tawi la Tower; kinyume na hapo mshiriki hataruhusiwa kuhudhuria kozi.

Jambo la Kuzingatia

Tafadhali zingatia kuwa gharama za safari, chakula na malazi zitagharamiwa na taasisi itakayokudhamini kwenye kozi. Ada yetu imejumuishia gharama za ufundishaji, gharama za utawala, viburudisho vilaini wakati wa asubuhi. Unatakiwa utoe taarifa kwenye ofisi zetu za NIP hapa Dar es Salaam kabla ya kuripoti kwenye mahali pa mafunzo.

Wasiliana nasi

Nyumba ya Maarifa, Mtaa wa Ohio

S.L.P 2021, Dar es Salaam, Tanzania,

Simu: (+255) 22 2110523/ 2126832/ 2126981 and (+255) 769 291905

Nukushi: (+255) 22 2128619/ 2126081

Barua pepe: info@niptz.org

Tovuti: www.niptz.org

